# MAFUNDISHO YA ROHO

## YA MT. MUTAWA WA JANGWA ISAAKA WA SIRIA

**MUFASIRI**
**MUTAWA DAMASKINOS GRIGORIATIS**

**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOXE**
**KOLWEZI CONGO**
**1990**

## FUNDISHO YA KWANZA

1.Woga ya Mungu iko mwanzo ya kila fazila. Woga inazaliwa na imani na inaoteshwa ku roho, ile inapenda kufanya kazi ya wokovu wake.

2.Mwanzo ya mutu kufanya uzima moja muzuri ni ya kusoma mafundisho kwa sababu hii sifa iko ya bure na haina sifa ya kweli.

3.Hakuna namna sisi kutosha kazi mbaya na zoezo mbaya ya roho yetu, bila nguvu na imani mbele ya Mungu wetu.

4.Kama tutapoteza neema ya Roho Mtakatifu wakati nyingi, basi tutakaa mapendo ya Mungu Mtakatifu.

5. Mwanzo wa uzima wa kweli iko woga mbele ya Mungu na hii furaha takatifu inazaliwa pamoja ndani ya roho zetu.

6. Watu wale hawapende vitu ya hii uzima na hawasikie sikitiko ya siku ingine, ndani ya roho yao inaotesha fazila ni kusema sauti ya Mungu.

7.Kama unapenda kusikia furaha na butamu ya maungano yake pamoja na Mungu ndani ya roho yako? Penda Mungu na watu wote.

8. Sawa vile maji ya kupenda kwa karatasi moja haiwezi kuzimisha hamu ya maji ya watu wote, njo vile na mwalimu moja hasiwezi kusaidia watu wengine kuokolewa paka kwa mafundisho yake, bila mufano muzuri.

9. Hii kazi muzuri ao mubaya inafanywa kwa hii uzima wako wote, ao Watakatifu wako wote hata mpaka kaburi yako; lakini hii kazi ya roho ulifanya pamoja na roho yako mtakatifu watakufata wewe kwa uzima wako wa milele.

10. Kama ulifanya kazi moja muzuri inafai kufichika kwa sababu ubatizo inakusaidia imani apana nguvu yako.

## FUNDISHO YA MBILI

1.Uso ya mutu wa unyenyekevu iko pamoja na kujishusha kwa uso ya Yesu Kristu.. Hakuna namna ya kuachana sisi mbele ya Mungu paka matusi, kucheka, zoezo mubaya na neno ya bure.

2.Inapasha kutakasa mwili wetu kwa sala na kazi muzuri, juu ya kuikala ndani yetu Yesu Kristu, katika Komunyo Takatifu.

3.Rafiki gani unapata ku mbinguni juu ya kukupokea wakati utatoka kwa hii uzima? Kwa shamba ngani unatumika juu ya kubeba malipo yako? Inapashwa kuliya sana juu ya Roho Mtakatifu kupumzika ndani ya roho yako atakasafisha uchafu yako yote.

4.Ee Bwana, ninakuomba na uniache mimi uniweke ndani ya shamba yako, unipe chakula ya mayani ya Watakatifu wa siri yako, unituliza, unifurahishe kwa furaha takatifu.

5. Hawawezi bila mapenzi ya Mungu kufanya kazi mbaya hata vitu vyote vya dunia, hata watu wabaya na nyama za pori. Mungu anawafunga juu ya kuishi mutu bila hatari.

6. Wale watu waliwafuata na majaribu mingi, Mungu Baba yetu anapenda kuwapatia hekima na neema yake!...

7.Mutu yule anapenda dunia asipende Mungu. Kila mutu anaishi pamoja na vitu hii ya uzima, hauwezi kuishi pamoja na Mungu. Yule anaangalia kwa macho ya roho yake vitu vya dunia, hasipende kuangalia vitu vya Mungu.

8. Mutu yule anapenda kabisa vitu vya mwili, anashusha mapendo yake kwa Mungu.

9. Mutu anapashi kuteswa kwa haki na afate mateso ya Kristu.

10. Inapaswa kujua ya kama bila majaribu uko mbali na Mungu hautembee kwa mapendo ya Watakatifu.

## FUNDISHO YA TATU

1.Watu wanachukia uzima ya masikini na Mungtu anachukia roho ya majivuno, kwa watu wa mali iko kitu kizuri, lakini kwa Mungu iko roho ya unyenyekevu na kusikia kosa yako na kulia.

2.Wakati unaishi kwa amri ya yesu Kristu ongolea majaribu. Ule mutu hasisadiki kwa Mungu, anaongopa tena kivuli yake. Kama mutu moja-moja anamwambia ya kama anatembea vizuri, yule mutu alipenda.

3.Amri yote ya yesu Kristu iko muzuri kupita zahabu ya dunia, kwa sababu yule mutu anafuata amri ya Yesu anapata Mungu ndani ya roho yake.

4.Kama mutu anaamini Mungu na ndani yake anamupenda. Ule mutu anawaza ya kama zambi yake iko kidogo, yeye atanguka katika zambi ingine mbaya sana.

5.Kila mutu anafata mapenzi ya Mungu, yeye eko na wasaidizi wa malaika wa Mungu. Yule mutu anavumilia ku unyenyekevu. Sauti ya chuki toka watu wengine, anafika fasi ya yulu kabisa sawa malaika wa mchanga!…

6.Ulipoteza uzima wako safi? Mungu anataka kazi yako ya wema, kama utaendelea na kazi yako ya usharati. Kama unapata chuki mbele ya mutu mwingine juu ya nini unakombana na kulala kidogo? Faida gani iko ya kulala kidogo, sawa vile unachukia ndugu yako?

7. Kama mazungumuzo na neno yako iko utamu, na watu wote watakuona sawa rafiki yao.

8.Ku majaribu yote utatusaidia kupata fazila na nguvu na imani, kwa sababu bila majaribu mafazila yetu yote iko ya uwongo na bure.

9.Kama tunasikia majaribu ya mutu moja ao fazila yetu, Bwana Yesu Kristu atabarikia juu ya kupoteza hii kitu na kupata unyenyekevu. Ule mutu anavumilia ku furaha kazi mubaya ya watu wengine; huyu eko na ulinzi wa Mungu.

10.Watakatifu wetu wanasikia nguvu kwa imanhi yao kwa ajili ya kuona ndoto na wanavumilia kwa majaribu yote katika mapendo ya Mungu.

11.Mutu yule anaacha moyo na uzima yake ku mikono ya Bwana Yesu Kristu anasikia ukimya kwa akili yake. Kama mutu hapende vitu ya hii uzima anapata uhuru wa roho yake na makelele ya akili yake anasimama. Hii ukimya ya mwili inaogoza kwa imanhi na akili.

12.Majaribu yote inasaidia kupata hekima ya Roho Mtakatifu, imani mbele ya Mungu inaleta nguvu ya kuzarau majaribu yote.

13.Pasipo sisi kuishi mateso ya Yesu Kristu hakuna maungano ya ma roho zetu pamoja na Mungu wetu.

## FUNDISHO YA INE

1.Kama mutu anasaidia watu weingine eko na furaha kwa Mungu.

2.Wagonjwa wanakuja kwa Mungu juu ya sisi kupata uzima wa roho yetu na mapendo ya Mungu.

3.Mungu anatuma kwetu sikitiko yote juu ya sisi kuja karibu Yake kwa sala, unyenyekevu na kutembea mbali na njia ya shetani.

4.Mambo ya mateso na sikitiko inatusaidia kwa kufata Mungu kwa ukweli na kutupa mambo yote mabaya inje ya hii neema ya uharibifu.

5.Iko namna sisi kupata uwezo mbele ya Mungu paka kwa sala na kwendelea. Roho ya wale watu wanaomba Yesu Kristu wanasaidia furaha na utulivu.

6.Yule mutu anatubu na anachukia zambi zake, atapata neema kwa Mungu.

7.Kama mutu anaishi kwa hii uzima sawa mufu, nikusema pasipo mapendo ya hii dunia, anavumilia furaha yote na majaribu na kazi mubaya. Kama mutu hafukuze zambi na zoezo yake mabaya ndani ya roho yake, anasirika, anatetemeka na anasikitika sana.

8.Neema ya Mungu inakuja karibu na mutu kwa unyenyekevu. Mutu wa majivuno watamupatia hali ya sikitiko juu ya kupata unyenyekevu na wokovu.

9.Mutu wa unyenyekevu anapokea saa yote wema na neema ya Mungu. Ee ndugu yangu, pata unyenyekevu mbele ya watu wote. Onyesha mbele ya watu wengine sifa yako na wote watakusifu. Hukumu mbele ya Mungu na utaona utukufu wa Mungu. Fanya nguvu ya kutazama watu wote na vilevile otasifiwa na atakutukuza Yesu Kristu. Inatoka sifa kwake. Kama mutu anafukuza sifa, hii ilimufata na inaonyesha muhubiri ya kujishusha kwake.

10. Kama mutu moja eko mupole, eko na uzima ya mwangaza na akili ya unyenyekevu, na anaishi sawa mutu bure, yule mutu eko: Kweli mtakatifu…Kama mutu anasikia njaa na hamu ya kupata Mungu na fundisho yake, Mungu atamujaza ndani ya roho yake na vitu vyote vya kiroho.

## FUNDISHO YA TANO

1.Penda kutembea na watu wa unyenyekevu kwa sababu uso yao na mafundisho yao italeta faida ya roho. Hapana kuepuka mutu moja mubaya atazarau watu weko na vidonda ya mwili. Sifu ndugu yako wa karibu kupita cheo yake na sema maneno muzuri ya vitu vile asione vilevile utamuponyesha katika zoezo yake mubaya!

2.Sopoka juu haufanye hamakia (controle) ya zambi ya mutu mwingine. Fazila ya mapendo, haisirike, haiofanye hamakia hatakuwa mtu mojua…

3.Kama unakataa hii ni mwanzo wa zambi, unamupatia shetani ruhusa ya kukombana na roho yako nguvu. Kama tunasoma Biblia Takatifu inatoka ya akili na mawazo yetu!…

4.Mambo ya kutenda zambi iko paka katika dunia, mambo ya kusirika ya kutakia matakio yote mubaya, ya kuchukia ao ya kupenda utukufu wa bure. Iko muzuri kupita kufa, mbele ya kuishi kwa hii uzima na tutafanya kazai mubaya.

5.Tosha zoezo mubaya ya watu wengine. Kama mutu anasungumuza na wewe unasema sauti hata moja unafanya zambi. Waza maungu yako. Kupita kidogo ya watu wengine. Epuka kuzungumuza neno ya bure pamoja na watu wote unawakutanisha weko na kula, kunywe kidogo vitu yote ya chakula na pombe. Epuka kutembhea bio-bio pasipo mambo yoyote. Wakati unazungumuza, sema mawazo yako ya utulivu na ukimywa bila kasirani, makelele na sauti mubaya.

6.Hauone uso ya huyu mutu ukonazungumuza naye pamoja, kama mutu moja anafanya kosa, hamutafanya hamakia ya hii kosa yake? Penda kufanya hii kazi ya unyenyekevu, kama uko mutawa, acha wazazi wako ku mikono ya Mungu. Vile utapata mapendo ya Mungu ndani ya roho yako. Rafiki wako ni watu wanaongoza Mungu. Iko mubaya wewe kufungula roho yako utaonyesha mambo na siri yako mbele ya watu wote. Ficha majaribu na onyesha paka mbele ya padri wa roho yako.

7.Pokea uzarau wako kwa watu wengine, lakini wewe kuzarau apana. Pokea watu wengine kukufanyia wewe kazi yasipo haki, lakini wewe usifanyie watu wengine kazi bila haki. Usipende watu wa dunia. Patia watu vitu vizuri, lakini ishi mbali ya watu wote. Epuka kusema saa nyingi kwa sababu saa nyingi iko ya wamaskini wa roho. Acha mambo ya kukombana na watu wengine. Toka mbali ya wale watu wanaishi kwa majivuno.

8.Haufanye uhamakia ya mafundisho ya makosa. Usitembee pamoja na watu wa kasirani, na kwa sababu itajaza roho yako kasirani ya azabu.

9.Uzaifu na sikitiko inaleta huzuni na shaka ku roho. Kama roho inafurahi haipende kuzungumuza kwa kinywa, hivi inafwatana na furaha ya roho na hali ya utamu. Hii furaha ya roho ni alama ya kufika roho yetu katika ufalme wa mbinguni. Hii furaha wakati inaingia ndani yetu inapatia roho uzima, inatutosha katika ngiza ya kipagano.

10. Hii kazi ya kusoma maneno ya Mungu, sala ya usiku inatuonyesha ya kama katika roho zetu ni mali na neema ya Mungu.

## FUNDISHO YA SITA

1.Ikala ndani ya nyumba yako na itakufundisha vitu yote. Vitu gani itakufundisha kuvukutu ya roho yako na itakwangazaa kwa machozi, kisha italeta ukimywa ya akili na hali safi ya akili yote. Fumbo ya Mungu kwa sababu hii yote anatupatia Mungu apaka kwa unyenyekevu.

2.Inapaswa kila mutawa kwa matendo na uzima wake wote kuonyesha mfano muzuri na kupatia watu wengine faida kwa sababu uzima ya Watawa ni tukufu wa kanisa ya yesu Kristu.

3.Kazi ya roho ya kila mutawa wa kweli ni:

Kuzarau vitu vya dunia.

Kula saa zote fasi moja ya ukimya.

Kulinda macho yake.

Kutosha mbali mambo ya maele kwa watu wengine.

Kuzungumuza sauti ya chini.

Kusihi kwa mayele kwa roho.

Kutoka mu watu wengi na kupitisha kusoma sala ya Mungu.

Kukataa sifa na kuvumilia nguvu majaribu yote.

Kulia saa yote, muchana na usiku.

Kuchunga uzima ya Bikira, kama anafanya hii yote anakuja karibu na Mungu na eko mwenye kufa mbele ya uzima.

1. Uzima ya roho iko na ma cheo tatu:
    a) Kwa cheo ya kwanza, watu wanaishi pale weko katika zambi.
    b) Kwa cheo ya mbili, wanafanya nguvu ya kutosha hii zambi na ubaya wao ndani ya ma roho zao.
    c) Kwa cheo ya tatu, watu walifika hii fasi walisikia neema ya Roho Mtakatifu sana.

5.Tutasema nini kwa yule mwaminifu, aliyebeba neema ya Roho Mtakatifu, ndani ya roho yake? Kama hastahiliwe kupata neema yote ya Mungu, kwa sababu anasikia hii wakati kwa uzima wake wote, ninasadiki ya kama huyu ataokolewa.

6.Neema ya Roho Mtakatifu inaanza kutembelea nyumba ya roho yako, wakati nguvu na akili yako inashuka na inabaki ndani ya roho yako.

7.Alama ya kukomea roho zetu ni alama gani?

a.Mali ya sala.

b.Kutosha majivuno katika maroho zetu na kukataa kujua zambi ya nfdugu zetu.

c.Kama tunapenda lufu letu na uzima wetu ku mbinguni.

d. Kama tunavumilia mambo yote katika furaha na sikitiko hii kwa uzima.

e.Kama tunashukuru na tunatukuza Mungu kwa mambo yote ya uzuri ni mubaya?

## FUNDISHO YA SABA

1.Yule mutu akili na roho yake iko paka mu kazi hawezi kuwa mutu wa ukimya na mwema, kwa sababu bila sala ya kwendelesha hakuna namna ya kufika karibu ya Mungu.

2.Mutu mwenye majivuno anatembea njiani na anajiwazia ya kama yeye peke eko yulu kupita watu wengine. Lakini kweli eko mutu mubaya kuliko watu wengine kwa sababu hapende kutembea mu njia ya Mungu hii njia ya unyenyekevu.

3.Wale watu wanatembelea watawa jangwani hawapate makelele, sikitiko na huzuni rohoni mwao.

4.Kazi ya kusoma Biblia saa yote inajaza roho ya mutu kwa ajabu na furaha takatifu.

5.Watawa jangwani wanalia machozi kila wakati kwa ajili ya sala na ya kusoma. Weko na machozi ingine kwani wanaongoza watu ku njia ya amani na akili na mafumbo ya Mungu.

6.Mutu yoyote atazarau utukufu wa dunia atastahili utukufu wa Mungu.

7.Kama mutu anamutii Mungu vitu vyote vitamutii naye vilevile, kwani amani inazaliwa rohoni mwake toka kwa Mungu. Kama tunakataa kujinyenyekeza Mungu atatupatia malipizi. Unyenyekevu wa kweli ni matunda ya majaribu na ya mambo ya Mungu.

8.Imani na fumbo ya komunyo takatifu inatupatia zawadi kubwa ya Mungu, na hii zawadi inasafisha roho zetu.

9.Watoto wadogo weko na mwili safi na roho yasipo zambi, akili yao ni safi. Kwa sababu ni paka na akili yetu kuiko namna ya kuangalia mambo ya ufunuo ya mbinguni.

## FUNDISHO YA MNANE

1.Sisi tuko namna ya kumufahamia Mungu katika inchi tunaishi, imani ya Mungu inapatikana humo, na matunda ya imani inakuwa nguvu juu ya kumjua Mungu rohoni mwetu.
2.Kama tutaweza kujua kazi gani ao mbaya, hii mambo inatuongoza ku imani ya Mungu. Imani inatuongoza kwa kumuogopa Mungu. Kumuogopa Mungu kunatusaidia kufika ku toba na ku yote kazi nzuri. Ku kazi nzuri kunatokea mambo ya kumujua Mungu Baba rohoni mwetu na kusikia mafumbo yenyi kuzaliwa toka mapendo ya Mungu.
3.Hii mambo ya kumuona Mungu ni mambo ya furaha saba kwa Mungu.
4.Unataka kupata uzima wa milele? Shika hii mambo mbili: Imani na unyenyekevu.
5.Wakati unaanza kuomba inapashwa kuangalia moyo wako kama kisuguu, buyoka, bilulu na bebe.
6.Umutolee Mungu mambo yako yote na omba nguvu mpaka ile wakati utasikia furaha rohoni mwako.
7.Ule mutu anapenda kufuata paka mafundisho ya dunia hataweza kupata kidogo na kusikia hii mambo na kazi ya Mungu. Inapaswa kukataa mafundisho ya bure ya hii uzima hivi atapata rohoni mwake mafundisho ya kujua na kusikia kweli Mungu Baba.
8.Ukipenda kusikia rohoni mwako furaha ya uzima wa milele, inapaswa uwe kama mtoto kidogo ndani yako, ni hivi inasema Biblia.
9.Kama utaacha mambo yako yote mikononi mwa Mungu, basi utaona matendo ya ajabu ya Mungu. Yeye anakupenda na anakusaidia daima.
10.Imani inatosha watu ku mabaya na ku mafundisho ya bure, basi inasafisha roho yetu na kisha tutasikia neema na furaha ya Roho Mtakatifu.
11.Neema takatifu inashukia yule mutu anayekataa masaidio na matumaini yote ya hii uzima na anapenda kufuata paka Mungu.

## FUNDISHO YA TISA

1.Fazaila ni ndogo kama mutu ni zaifu na anapenda usingizi.

2.Wakati mutu anajivuna mingi, Mungu anatuma ku maisha yake majaribu mengi sababu ya kumushinda sababu ya kupata njia ya unyenyekevu na kuomba mara ingine saidia takatifu.

3.Mutu fulani anaishi kama mufu katika hii uzima wakati hasikitike juu ya mambo ya hii uzima wala anafurahi kwa vitu vyote venyi kumufurahisha.

4.Unasema nini ee mutu? Unapenda kupanda mbinguni, kuingia katika ufalme wa Mungu na kutuliza roho yako kwa kuungana pamoja na malaika wa Yesu Kristu na uzima wa milele na unauliza kama hii njia iko nguvu.

5.Kama roho  yetu inapenda sana mambo ya Mungu, basi mwili wetu hautazungunika sababu ya matendo mabaya, kwa sababu inaongojea kitu moja kubwa: Ufalme wa mbinguni.

6. Unyenyekevu ni nguo ya Mungu!...Hii mavazi anavaa Mungu Yesu Kristu na inaingia rohoni mwetu katika zawadi yake, mwili na damu yake, na anatutakasa.

7.Mutu munyenyekevu hakuna mutu mwingine kumuchukia wala kumuzarau ao kumugombanisha. Anapenda Kristu na watu wote wanamupenda. Huyu mutu wa unyenyekevu anapenda wote na wote wanamufuata. Kila mutu wa akili na kila mwalimu wanafunza kwanza kwa mutu munyenyekevu na wanashika neno lake. Neno lake ni tamu kupita sali na mushumaa. Watu wote wanamuona kama Mungu na hakuna hata mmoja atamuzarau na kuzarau uso wako. Kama mutu mmoja anamuzarau huyu munyenyekevu anachabula Mungu Yesu Kristu. Wa nyama kali wa pori wanakaa karibu yake bila mambo ya makali kwa sababu wanasikia kwake manukato ya Adamu!…

8.Mutu munyenyekevu anasadiki ya kama ni paka yeye peke yake eko mubaya na mwenyi kustahili kuzaraliwa kwa wengine. Anashika nyoka kama nzige! Akikuja kwa watu wanamwogopa kama yeye ni Bwana yesu Kristu! Alafu nguvu ya shetani inaharibika mbele ya wanyenyekevu! Hii ni utukufu ya fazila ya unyenyekevu na hii fazila watakatifu wote wa kanisa yetu wanaipokea.

9.Kuiko namna kwa kila mutu kuwa munyenyekevu? Ndiyo, paka na nguvu ya Komunyo takatifu na ya fazila zote walipata Mitume wa Bwana yesu Kristu siku ya Pentikoste.

10.Heri yule mutu alijuwa matendo yake mabaya na kuyacha, kwa sababu huyu aliweka msingi wa fazila zote.

## FUNDISHO YA KUMI

1.Kama mutu hanguke katika majaribu ya roho na ya mwili, hawezi kujua ya kama yeye ni mwenyi zambi. Basi, mutu akianguka katika zambi, ataanza kumuomba Mungu na unyenyekevu na sikitiko ya roho yake.

2.Majaribu ya roho ni hii: Kukosa imani, matusi, majivuno, kushindana na shetani, hasira na taabu. Majaribu ya mwili ni hii: Magonjwa ya mwili; na hii mateso watu wanaivumilia kwa ajili ya mapendo ya Mungu.

3.Mungu anapenda watu wanyenyekevu kama anavyowapenda Malaika na Waserafi.

4.Wakati mutu anajishusha anajaa neema ya Mungu na roho yake inajaa na furaha. Basi asifanye sala kwa nguvu, lakini kwa furaha.

5.Kama tunapokea Komunyo takatifu Mungu wetu anakuja karibu nasi kwa zawadi yake na asinyanganye neema yake kama sisi tunaichunga na unyenyekevu.

6.Ule mutu asijue mambo ya kosa yake, hana unyenyekevu. Mutu asiye munyenyekevu hana na fazila ya Mungu. Mutu kama hana na uzima wa hulu sana, anaogopa kwa sababu hamutumainie Mungu. Mungu anatupatia majaribu paka kwa ajili ya mapendo yake.

7.Ule mutu anapenda kumufuata Mungu eko na matumaini na hekima kwa Mungu.

8.Ule mutu mwenyi kuishi katika zambi hana na namna ya kupata matumaini ya Mungu kumusaidia kama anapatikana na mambo ya mateso mbele ya kutubu kweli.

## FUNDISHO  YA KUMI NA MOJA

1.Hautake kukamata pepo ku mikono yako, nikusema imani bila kazi;

2.Sopoka katika uzima wako. Nguvu ya kazi ya Mungu na amri yake inaenda mbele na kisha kunafuata matumaini kwa Mungu. Kama unaamini, unafanya muzuri, lakini imani inataka kazi na matumaini mbele kwa Mungu inaonekana paka kama tunateswa kwa kupata fazila kwa Mungu.

3.Mungu manatuaambia hivi: Mimi ni karibu yako katika mateso na huzuni yako juu ya kukusaidia na kukutukuza na kukuonyesha wokovu wa roho yako.

4.Roho yenyi kumupenda Mungu inafurahi paka kwa mambo yote ya Mungu, inapaswa kuondoa rohoni mwako hii mambo yote ya uzima wa dunia.

5.Kama mutu mmoja anasema maneno mengi anataka kusikia maneno mengi ya watu wengine yenyi inazunguusha macho yake fasi yote, na wakati tena yeye ni mgonjwa, huyu mutu hatasikia neno hata moja nzuri utalomuonyesha rohoni mwako.

6.Hii kazi tunafanya kwa ajili ya Mungu nyuma italeta furaha. Kwa furaha uvumilia mambo yote ya wewe kuzarauliwa hivi utakuwa na uwezo kwa Mungu. Ule mutu mwenyi kuzarau sifa ya bure ya hii dunia anasikia rohoni mwake utukufu wa uzima wa milele.

7.Ukiwasamehe wengine makosa yao waliokukosea, ni fazila kubwa. Mara ingine inapaswa kuvumilia ujeuri wa watu wengine hivi utawasaidia wale watu walioshindana nawe.

8.Sifu sala ya usiku ku kazi ya roho na utapata utulivu rohoni mwako. Fanya nguvu ndani yako ya kusoma kimya Biblia takatifu utashangaa maajabu ya Mungu wetu. Chunga roho yako ku kosa ndogo sababu usianguke katika kosa kubwa. Mutu mwenyi kuomba utukufu wa hii dunia hayuko munyenyekevu.

## FUNDISHO KUMI NA MBILI

1.Mutu musharati hana na akili ya unyenyekevu na roho safi, anakula chakula cha nyama ya pori apana chakula cha malaika...Munyenyekevu eko na nguvu katika uzima wake; mutu mwenyi majivuno ni mutumishi wa usharati.

2.Kufundisha mambo ya Mungu ni kazi nzuri lakini kusafisha moyo wako kwa ajili ya mapendo ya Mungu ni vizuri sana.

3.Mbele ya kusafisha roho zao watu wengi walienda duniani juu ya kusafisha roho za watu wengine lakini walipoteza roho zao kwa sababu mawazo mabaya yanapatikana rohoni mwao na wakafa katika roho.

4.pahali unapokwenda shika mwili wako kama mugeni hivi utachunga roho yako ku mambo ya nguvu. Kwa kila mambo sadiki haujui kitu hata moja.

5.Zungumuza kama mwanafunzi apana sawa mwalimu. Kwa kila mambo inapaswa kusadiki ya kama uko na lazima ya kusikia fundisho hivi utakuwa mutu mwenyi akili mingi katika maisha yako.

6.Acha kusoma vitabu vya mafundisho ya uwongo, soma paka vitabu vya mafundisho ya kanisa yetu.

7.Bariki kusoma watu wengine na apana kuwafinga kwa sababu baraka inazaa baraka ingine na neno la chuki litazaa chuki ingine.

8.Usiwafundishe wengine fundisho lile wewe haukufunza.

## FUNDISHO KUMI NA TATU

1. Wakati neema takatifu itafungua macho ya roho yako, machozi yako itanguka kama chemchem, na hii machozi hi alama munene yenyi kuonyesha ya kama Mungu anatembelea katika neema yake.

2.Soma Evangelio Takatifu katika fasi ya ukimya hivi utajuwa mambo yote ya ajabu ya Mungu na roho yako itafurahi na furaha ya mbinguni na hali nzuri.

3.Pokea nyumbani mwako wale watu wenyi mufano nzuri pamoja na fazila.

4.Unganisha pamoja sala yako na kazi ya wema hivi utangazwa na mwangaza takatifu ya Mungu.

5.Soma Biblia takatifu na uzima wa mapadri watakatifu wetu hivi utasikia furaha ya Mungu kupita wakati utaanza kufanya sala.

6.Kama vile kahaba moja hazungumuzake mambo ya uzima safi (morale) vile vile na watu wa shetani jawawezi kuzungumuza mambo ya kiroho, kwa sababu hawapewe ndani ya roho yao baraka na utamu wa kazi ya roho.

7.Bwana Yesu Kristu alikula pamoja na watoza kodi na wenye zambi juu ya kuwakokota kwa kuwa na woga wa Mungu. Wakati unafanya kazi moja vizuri unaongojea kupata malipo, lakini Mungu wetu atakupa.

8.Mutu yule hana na vitu vya kula anachunga vizuri uzima wake. Kama akiwa na chakula yote hawezi kutembea vizuri katika maisha yake. Kama mutu anashindana ku nvita mbele ya mambo ya zambi, anafanana sawa yule mutu anafunga milango ya muji anagombana na adui wake ndani.

9.Kazi ya mikono, ilituonyesha wa Padri wetu paka kwa watu kidogo weko na fazila ya Mungu. Wale watu wanaishi uzima moja ya roho yulu kupita watu wengine kazi ya mikono inapata makelele.

## FUNDISHO KUMI NA INE

1. Kama mutu moja anakaa nyumbani kwa ukimywa akifanya sala kwa Mungu, hii kazi yake ni zawadi ya Mungu.

2.Kama mutu anazarau kazi yote ya zambi na anafanya kazi ya fazila eko na namna ya kupata matumaini ya wokovu wake atastahili neema takatifu. Yule mutu alipata fasi ya yulu kabisa kwa fazila ya yesu Kristu, alipata katika roho yake fumbo ya furaha ya milele.

3.Kama mutu hapende kwacha kuacha mambo ya zambi na mawazo mbaya ndani ya roho yake, hakuna namna yeye kupata ushirika nzuri ya Roho Mtakatifu...

4.Heri mutu yule anakaa kwa ukimywa na anafanya ya Mungu na hapende kutumika kazi ingine ya bure....

5.Kama mutu anakaa katika dunia hii lakini anageuza uzima wa roho yake, kweli atapata katika roho yake fumbo ya furaha ya milele na alistahili kuwa na neema takatifu.

6.Alama ya mapendo ya Mungu ni hii:

Uso inafanyika sawa mwangaza na iko na furaha.

Mwili inasikia kivukutu.

Mutu huyu anaongojea lufu kwa furaha.

Anakumbuka saa yote mambo ya mbingu na anasungumuza bure.

Akili ya mutu yule ni ya juu na anasungumuza pamoja na Mungu.

7.Kama hatupate fazila ya unyenyekevu, hatutasikia furaha rohoni mwetu, wala hakuna namna nguvu ya shetani kutoka adui yetu.

8.Wale watu weko na mapendo ndogo na hawawezi kupata uzima wa milele, Mungu anangoza roho yao kwa kupata fazila ya uzima.

9. Inapashwa kujua ya kama, kama una lazima ya kitu kimoja, hii kitu itaishi na itabaki rohoni mwako.

## FUNDISHO KUMI NA TANO

1. Wakati Mungu analeta mateso katikati ya watu inatuonyesha mara moja mapendo yake. Kama mutu moja hawezi kuvumilia mateso ya uzima, ndani mwake anaishi na zambi ya dunia. Rohoni mwake munaishi mapendo ya mwili lakini hayuko mapendo yaq Kristu....

2.Wakati mwili wetu unateswa na majaribu na sikitiko, inakosa mapendo ya Kristu.

3.Njia yenye kuongoza kila mutu ku mwangaza na uzima katika Kristu ni:

Ukimya.

Kula chakula chenye kuenea.

Kusoma saa fundisho ya Mungu na kazi ya Mungu, nikusema: Komunyo Takatifu, Sala kwa Mungu, kusoma na kusikia maana ya Biblia. Tukifanya hii yote uzima wetu utapata uhuru kweli wa Kristu, furaha ya roho na utulivu ya roho pamoja na Yesu Kristu katika ufalme wa mbinguni.

4.Mutu akikula chakula mingi na mara mengi, anasikia:

Kizunghuzungu kichwani.

Mwili yake ni uzito na anaregea.

Mawazo ya akili yake inafata giza.

Ni muzaifu ku kila kazi ya roho.

5.Tunakataa kusoma Biblia Takatifu kwa sababu hatujue uzuri wa neema ya Mungu. Kwa ajili ya ugonjwa wa roho.

6.Mutu mwenye kuishi ao kukaa katika jangwa hana na majaribu ya nguvu, kwa sababu haone wanawake, wala hasikie mazungumuzo yao mbaya, wala kitu ingine juu ya kuharibu uzima wake!..

## FUNDISHO KUMI NA SITA

1.Shetani wa kwanza anatuonyesha kuacha sala ya roho kwa Mungu na hii kanuni ya sala alitupatia padri wa roho yetu, vile anatuangazusha ku kazi mbaya kabisa.

2.Mutu atakuwa na roho ya nguvu kama eko na imani kwa Mungu na hii imanhi inapata unyenyekevu ku roho.

3.Mutu atakuwa na woga mara mbili:

Kwa sababu anapenda mwili wake kupita vitu vingine.

Ka,a eko na imani ndogo rohoni mwake. Akishinda hii yote mbili, ataamini Mungu wa kweli.

4.Uwezo kwa Mungu unapatikana toka moyo nzuri na ku kazi ya fazila.

5.Ukikaa kimya bila kuzungumuza nikusema una mambo ma tatu:

Ao juu ya kupata utukufu bure ya watu wengine.

Ao kwa ajili ya mapendo ya uzima wa kweli.

Ao kwa sababu uko na kazi moja kimungu ndani ya roho yako.

6. Mungu na wa malaika hawafurahi ku sikitiko na mateso yetu, lakini shetani anafurahi wakati sisi tunapumuzika. Wakati tunakataa hii sikitiko na mateso ya uzima hii, tunakataa Mungu Baba yetu, kwa sababu mateso na sikitiko hii haitusaidie kweli sisi kupata njia ya fazila.

7.Sikitiko na mateso inauua zambi na mawazo yetu mbaya.

8.Kama mutu anasoma usiku na jua mafundisho Takatifu pamoja na sala ya roho anafanana sawa na kula Sali.

9.Ule mutu anatupatia nguvu ya kufanya sala kwa Mungu atastahili kupokea zawadi kubwa ya Roho Mtakatifu kwa Mungu.

10.Kama kazi yako ya jua inasikilizana pamoja na kazi ya usiku, basi utakaa daima katika mikono ya Yesu Kristu. Hii kazi ya roho haitaharibika kila siku kama unatumika nguvu.

## FUNDISHO KUMI NA SABA

1.Wakati ninaomba kwa ukimya mbele ya Mungu na ninasoma Biblia Takatifu, machoni mwangu munafanyika chemchem mbili ya machozi.

2.Toba ya kweli italeta unyenyekevu na kisha hakuna mawazo ya usharati.

3.Mungu anahurumia zambi yote, bila hii zambi hakuna toba. Watu wingi wanapokea baraka ya Mungu, ole wake yule mutu anakataa kumushukuru Mungu katika uzima wake.

4.Kama unapenda kuvumilia sikitiko yako ndogo, inapaswa kuwaza bila sikitiko munene, ni hivi wanavumilia watu wengine.

5.Pata imani mwilini mwako, hivi mbingu na inchi itakuwa na amani kwako. Fanya nguvu amani ingie ndani ya roho yako na utaona mbinguni.

6.Hii furaha ya roho haina pamoja na furaha ya vitu vya dunia. Mambo ya kusikia ufalme wa mbinguni ndani ya roho yetu ni paka na ushirika wa Roho Mtakatifu, na hapana mkwa vitu vya bure.

7.Mutu mwenye penda fazila ni yule mwenye pokelea furaha ya kazi mbaya yenye fata fazila.

8.Utafanya nguvu kusoma Biblia Takatifu juu ya kufukuza mawazo mbaya. Kama mtu moja anakosa, wewe unapaswa kumusaidia juu ya yeye kusikia nguvu na wewe Mungu atakuhurumia.

9.Akili ya mutu asiye penda kuwa na imani na sala rohoni mwake, kwa sababu msaada wa Mungu unakimbia ndani na inamuingia pepeo muchafu.

10.Zawadi ya Mungu inakaa kwa mwenye kuwa na roho safi.

## FUNDISHO KUMI NA MNANE

1. Nini yenyi kuleta mateso duniani:

Kupenda sifa na kuchukia watu wengine

Kupenda mali.

Furaha ya mwili.

Utawala.

Majivuno na furaha ya hii uzima.

Tukiacha hii zambi yote mbaya, basi tutakuwa watu wenyi uhuru na tutapumuzika na pumuzi ya Roho Mtakatifu, hivi tutakuwa watu wa roho.

2.Furaha na sala ni zoezo kwa wenye kufuata uzima wa Kristu. Mambo ya kuangalia vitu vya mbinguni ni kazi ya wale wenyi kufikiri juu mbinguni, kwa akili na roho yao.

3.Namna yote ya maombi na mufano wa kupata sala safi. Inje ya hii sala hakuna ingine. Paka mmoja katikati ya elfu moja eko na namna ya kupata sala safi.

4.Amuri yote ya Yesu Kristu inasaidia roho yetu kuwa safi.

5.katika uzima wa milele Watakatifu hawafanye sala. Wanafurahi na wanakaa wote pamoja, katika hii utukufu Roho Mtakatifu aliwapatia.

6.Mambo nini kama mawazo ya mutawa mmoja mukubwa inatoka juu? Ni sala ya akili ilipanda mbinguni naye hasisikie mwilini mwake.

7.Wakati padri atatayarisha roho yake na ataanza kufanya sala atasopoka na akili yake juu asiwaze mawazo mbaya, kwaki Roho Mtakatifu anashuka katika mukate na vinyo zenye kupatikana pa Meza Takatifu kwa kuitakaswa.

8.Maonyo yote ilionekana kwa watu wakati ilifanyika asla mbele ya Mungu.

9.Heri ule mutu mwenye kutoa sala ya safi, nikusema akili yake itabaki pasipo mawazo ao mazuri ao mbaya. Natumainia kufika na sisi ku hii mwendo ya roho pamoja na Neema ya Yesu Kristu.

## FUNDISHO KUMI NA TISA

1.Kama tunasoma siku yote Mafundisho Takatifu roho yetu itaangazwa tena atakaa safi pasipo zambi.

2.Malaika Watakatifu wanabeba uso ya watakatifu fulani na wanakuja katika ndoto, kila muchana na wanapita na mawazo mazuri na wanaleta furaha na utulivu.

3.Kama mutu mmoja kila siku eko katika akili yake mawazo mubaya ya usharati, ile wakati ya kulala shetani anakuja na anakuhuzunisha roho yake.

4.Roho inahuzunika na inaregeza zaidi kama inapata mawazo ya bure yenyi kutoka inje, na kama mutu anakataa kupokea Komonyo Takatifu na kufanya sala.

5.Kazi ya Mutawa si kuwapokea watu nyumbani mwake na kuwapa chakula, sala ni nzuri kabisa mbele ya kila kazi ya wema, hii ni kazi ya watu wa hii dunia.

6.Kama wakati wa sala akili yako iko inje, anza kusoma Evangeli Takatifu na acha sala. Kazi ya kusoma ni chemchem ya sala safi.

7.Kama unasikia furaha wakati wa sala kwa Mungu, fanya sala yako yote vile. Kama unatosha machozi, acha kufanya sala yako…

8.Majivuno inaleta zambi ya usharati tena majivono in aleta mawazo ya uongo.

9.Fazila inapenda ukimywa. Ukimya inazaa furaha ya machozi mengi rohoni. Ukimwa ni yulu kabisa ya kazi ingine yote ya uzima wa Mutawa.

10.Mapendo ya Komonyo Takatifu inatuliza mwaminifu fulani ku mateso na sikitiko yake, anayopata katika hii uzima.

11.Ule mutu anapenda sala ya Yesu Kristu, anapenda na uzima ya jangwani kwa sababu ni kule anapata Kristu na kuzungumuza naye. Kama mutu ni rafiki wa hii dunia, anapenda kupatikana katikati ya watu wengi.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI

1.Kama mutu moja anasikia rohoni mwake mambo ya zambi zake iko yulu yake ule mutu anaweza, kwa sala yake, kufufua wafu!…Huyu mutu analiliya hata saa moja zambi zake, eko yulu kuliko ule mutu anasaidia watu wote na mafundisho yake! Kama mutu moja anamufuata Yesu Kristu na sikitiko yake kwa ajili ya zambi zake eko yulu kupita mutu wowote mwenye kutukuzwa na watu wengine.

2.Ni lazima kukumbuka lufu yetu ivi tutachekelea vitu vyote vya bure vya hii dunia, vilevile tutastahiliwa uzima ya Paradizo.

3.Vitu vyote vya hii uzima vinatupatia makelele kama tunapenda kuzungumuza na Mungu tutasema hii sala: “Bwana yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi”, hivi tutapata mapendo ya Mungu na furaha ya milele!…

4.Wale wanapenda uzima ya zaifu, hakuna namna Roho Mtakatifu kufika rohoni mwao, lakini paka roho ya shetani. Watumishi wa kweli wa Mungu wanaishi na sikitiko na mateso moyoni mwao, lakini watu wa hii dunia wanapenda usingizi na furaha ya bure. Waaminifu wa Mungu wanaliya kwa ajili ya zambi zao na ya watu wengine, na watu wa hii dunia wanacheka. Watu wa Mungu wanachunga kifungo ya chakula, lakini watu wa hii dunia wanafurahai na furaha ya mwili.

5.Kama tunapenda kufuata amuri wa yesu Kristu, tutapata mu uzima yetu sikitiko na majaribu mengi na chuki ya shetani. Kwa kuvumilia inafaa unyenyekevu na kisha tutapokea neema ya Mungu.

6.Mungu hapatie mutu moja malipo ya roho, kwa sababu yeye eko na fazila yake, lakini paka ya unyenyekevu wake. Bila unyenyekevu wote ni bure.

7. Yesu Kristu hapende kwanza kazi juu ya amuri yake, lakini anapenda kila mutu kutayarisha roho yake sababu aokolewe.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA MOJA

1.Kama tutaacha mu kazi zetu na kufanya sala kwa Mungu haitaleta majivuno katika uzima wetu. Ni vile malaika Mulinzi anatoka rohoni mwetu na shetani anaingia rohoni mwetu.

2.Kama unapenda kuwa na zawadi moja ya Mungu, inapaswa kumuomba Mungu uwe na mambo hii:

Kujishusha.

Uwe na malaika Mulinzi.

Kama roho yake itapata majivun, omba kwa Mungu akutosha hii zawadi.

3.Juu ya kutosha majivono ni lazima kulia na kusikitika juu ya kupata unyenyekevu, na zawadi ya Mungu inaleta uneynyekevu kwa watu wote waishi ndani mwake.

4.Mbele ya kusikitikia zambi rohoni mwako muna majivuno. Mbele ya zawadi ya Roho Mtakatifu kufika rohoni mwako unyenyekevu inatangulia kuingia.

5.Majivuno haiko wazo moja itaingia wakati kidogo ndani ya akili yako. Ni hali moja isiyojulikana hata kidogo. Mambo gani ya kusikitikia zambi yako.

6.Kama mutu anamupenda Mungu zaidi sana hatapenda kukaa mu hii uzima, atapenda kufa.

7.Kuvumilia mara nyingi inaongozwa kwa unyenyekevu. Unyenyekevu unaleta afya ya roho zetu. Afya ya roho yetu inaleta mambo ya kumujuwa Mungu Baba yetu. Mambo ya kumujuwa Mungu inaleta mapendo mbele ya Mungu. Mapendo ya Mungu inatuletea furaha, na hii furaha ni utamu sawa Sali.

8.Uzima wa milele ni mambo ya kusikia Mungu ndani ya roho yetu. Hii mapendo ya Mungu ni yulu kupita furaha ingine.

9.Mutu yule ataopenda vitu vyote vya dunia na anachukia utukufu wa Roho Mtakatifu ana na unyenyekevu wa kweli.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA MBILI

1.Kama mutu anastahili kupata rohoni mwake neema takatifu afukuze mawazo na zambi zote isiingie ndani ya roho yake, kwa sababu ndani muna nguvu zingine kupita matakio, nikusema mapendo na furaha ya Mungu.

2.Kama mutu anazunguka na vitu vya dunia hii, akili na roho yake anaharibika hawezi kupata uzima rohoni mwake.

3.Ewe Bwana Yesu Kristu unisaidie kuchunga na nguvu roho yangu katika dunia hii. Lufu na zambi ni kwa yule mutu asiyependa hata kitu moja ya uzima hii.

4.Wakati mutu moja anapata baraka ya kuungama, anaanza kusikia katika utukufu na neema utamu wa uelekevu wa Roho Mtakatifu.

5.Hii mapendo ya Mungu tunaisikia sana moto katika roho zetu inauunguza zambi yetu ya roho na mwili. Kama mutu anatumika na sala na kusoma anasikia ya kama anaishi inje ya hii dunia na vile atapokea zawadi ya utukufu na vitu vya ufunuo.

6.Adamu, Eva na nyoka walifanya (kutenda) zambi. Lakini mafingo ya Mungu ni ya kwachana kwa kila mmoja. Kwa hivi kila mtu, kama anatenda zambi atapata mateso miongi katika Hadeze.

7.Mutu yule anashindana na shetani, wakati ataanguka ku zambi moja, atalamuka na ataendelea na mashindano yake. Lakini mutumwa wa zambi anatafuta namna juu ya kupata furaha ya zambi na asimame kutenda zambi zingine.

8.Kama tunauzaifu kwa ku sali na kusoma Biblia Takatifu na vitabu vingine na tunakataa kupokea Komunyo Takatifu, basi shetani atakuwa ndani ya roho sawa sultani mkubwa.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA TATU

1.Kama sisi tuko watawa wa zambi, roho yetu ni uzaidu.

2.Mutu wa kimya anafafunua siri ya Mungu. Mutu yule anasema mengi na ya bure eko mbali na Mungu.

3.kama mutu anachunga roho yake, bila mashimango na kuhukumu wengine hana namna ya kumuona Bwana Mungu wetu na kufukuza shetani.

4.Inafurahiwa roho ya mutu yule anafanya nguvu ya kusaidia roho yake.

5.Sawa vile samaki akitoka inje ya bahari anakufa, vilevile akili yetu wakati inatoka kwa Mungu inakufa.

6.Kusali kwa Mungu ni namna ya kutosha zambi zote na zoezo mbaya.

7. Kama hakuna uzima safi katika roho yako, katala zambi mbaya na usisirike. Mbingu itafika ndani yako na utaona Kristu Mwokozi na malaika zake.

8.Mutu yule wakusirik, kasirani, kupenda utukufu wa bure, vitu vya bure, chakula nyingi, anazungumuza na watu vibaya, eko na majivuno, roho mbaya moyoni mwake munajaa zambi nyingi, kwa mutu yule anatembea katika ngiza.

9.Kama mutu anajinyenyekeza kwa Mungu Bwana yesu Kristu anamuongezea hekima na akili mingi.

10.Kama tunakutaa utulivu wa hii dunia, tutastahiliwa utukufu, furaha katika Roho Mtakatifu.

11.Kama mutu anawarafiki watajiri awe masikini mbele ya Mungu.

12.Kama mutu anakumbuka lufu yake na, anachunga mwili wake bila kutenda zambi, Roho Mtakatifu na Roho ya Mungu itazaliwa rohoni mwake, itamupa furaha na ukimya.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA INE

1.Mutu yule wa roho safi, anasungumuza daima mambo ya roho. Lakini mutu yule anaishi katika zambi anazungumuza mabaya tena anasema rohoni mwake mabaya.

2.Usizungumuze bure na watu wengine, inafanya roho zetu kuwa nzito na mwangaza wa Roho Mtakatifu inatoka ndani mwake.

3.Kama mutu anafanya nguvu kufanya sala kwa Mungu anakula ngombe mwenye kunona (Luka 15,23). Penda Mungu juu ya wewe kutoka katika mapendo ya dunia hii.

4.Mutu yule anatayarisha kila wakati karamu sababu ya kula ni mutumishi wa shetani, na roho yake inapata zambi ya mwili.

5.Matunda ya zambi ni: Vinyo, wanawake na kuwa na mali...

6.Mwenye kuwa maskini kwa Mungu anapata mapendo na zahabu ya roho.

7.Furaha ile anasikia mutu yule anaomba kwa Mungu ni tamu kuliko furaha ingine ya chakula ya ngombe na harufu ya manukato.

8.Heri mutu yule mwenye kula Mukata Takatifu iliyoshuka mbinguni na ilileta uzima dunaini, nikusema Komunyo Takatifu. Inaleta furaha kwa yoyote mwenye kuipokea saa zote.

9.Heri mutu yule anasikia rohoni mwake utamu ya uzimja wa kweli, nikusema Roho Mtakatifu kama anakunywa maji hii neema ya Mungu, roho yake itajaa na furaha siku zote.

10.Mutu munyenyekevu na mupole anapendezwa na watu wengine, bila chuki na majivuno ya watu rohoni mwao.

11.Malaika Watakatifu wanatupenda sisi kama ndugu, wakubwa wetu wanapenda wandugu zao kidogo.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA TANO

1.Kuvumilia na ukimya inatusaidia kuungana pamoja na Yesu Kristu katika sala yake.

2.zarau kazi ya ovyo juu ya kupata vitu vya sifa. Ishi sawa mufu katika roho yako, juu ya kusihi milele.

3.Acha kazi ndogo ya ovyo juu ya kupata matendo mazuri na makubwa usifanye kuwa mufu mbele ya hii uzima kisha utaishi lufu! Penda kufa na hapana kusihi pasipo kazi ya roho. Tafuta hii vitu ya faida na sifa ya roho yako, sawa vile walifanya Solomoni na Heliseo na vile utatukuzwa mwili chini na kule mbinguni.

4.Kuna mutu anaomba katika sala yake vitu vya ovyo ya dunia hii, anamutukana Mungu. Kama mutu moja anazarau mwili wake na anakataa zambi ya mwili atapata furaha kwa wa malaika.

5.Kama uko na hamu ya mapendo ya Mungu, yeye atafurahi kwa mapendo yake na kisha atakupatia neema yake!

6.Kama unaomba kitu moja kwa Mungu naye hakupatie, anafanya vile kwa sababu haustahili kupata kitu ile unaomba: Hauombe na nguvu katika roho yake na haufike wakati huu wa kupokea zawadi unastahili kuomba.

7.Mutu yule mwenye kuwa na vitu vya dunia hii hawezi kupata vitu vya kule mbinguni na hakuna namna ya kuipata hata kidogo.

8.Uwe na akili nzuri, uzima na upole juu shetani na majivuno yake isiingie rohoni mwako. Penda unyenyekevu kuliko matendo yote.

9.Kama unafukuza mateso na sikitiko rohoni mwako utapata uzima kwa sababu katika hii mambo yote utamuona Mungu. Bila majaribu hatuwezi kuingia katika ufalme wa mbinguni.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA SITA

1.Fanya sala ya uepushe uzima wako katika majaribu hii:

Kutokuamini.

Matusi.

Majivuno.

Majaribu ya shetani na

Kasirani.

2.Mwili inapaswa kuvumilia hii mateso:

Magonjwa.

Mateso kwa ajili ya kumupenda Bwana Yesu Kristu. Kwa mateso katika hii uzima tuamini wema wa Mungu ili tuwe na uwezo wa Mungu, hekima. Hivi tutajua namna ya kupata mapendo ya Mungu…Kwa majaribu mengi Mungu anapima mapendo yetu kwake.

3.Juu ya kupata fazila inafaa mbele kupata majaribu mengi. Bila kuvumilia ku hii majaribu hakuna namna ya kupata fazila ya Mungu hata moja.

4.Kama mutu moja anaacha uzima wake safi, ao atatosha imani ya Kristu rohoni mwake ao kwacha fazila takatifu, mwisho yake atapoteza imani yake na wokovbu wa roho yake.

5.Neno la Mungu ni tamu kabisa kupita sali na ni sawa maji ya chemchem inayofurahisha roho ya mutu.

6.usiombe shauri kwa mutu mwenye kuwa na mifano mbaya hata kama ni mwenye akili mingi.

7.Mungu hawezi kukupatia zawadi bila kupata majaribu.

8.Kama unatembea vizuri katika uzima wako wa roho, hautapata majaribu mu uzima wako, kama Mungu anakuja neema takatifu.

## FUNDISHO MAKUMI MBILI NA SABA

1.Ulizo ya kwanza: Majaribu inafika ya kwanza ao zawadi? Ao zawadi njoo inafika ya kwanza kisha majaribu inafuata?

Jibu: Mituma Watakatifu wa Bwana jambo ya kwanza walipokea Roho Mtakatifu na kisha walifika mu dunia ya zambi (majaribu). Mungu anapenda kazi moja muzuri kisha kunafuata sikitiko. Neema Takatifu inatembea mbele lakini haionekane bio-bio ku matunda na kazi yake.

2.Kama mutu moja anawaza ya kama ni mwenye akili na mkubwa, kweli ataanguka kama majivuno yake ni mengi, katika majaribu hii:

a) Atapoteza heshima yake.

b) Mawazo mengi ya usharati itafika kwake.
c) Azabu na makelele itafika kwake.
d) Kutukana Mungu.
e) Mazungumuzo ya neno la ovyo.
f) Atapoteza ulinzi wa roho yake na matumaini na imani.

3.Kama Mungu anataka kusikitikia sana mutu mmoja kweli atamwacha ajaribiwe:

a) Kuhuzunisha moyo.
b) Kutenda kazi sawa wa mazimu. Hivi vyote ni
c) Matunda ya majivuno. Lazi ya kuponya ni jambo la unyenyekevu...

4.Unyenyekevu unatosha nguvu ya majivuno na toka hii fazila kuna kuwa kuvumilia kwa watu. Tunda la kuvumilia ni utulivu katika na toka hii yote kunakuwa mapendo ya Mungu. Ni vile inakomea furaha ya Roho Mtakatifu na huyu Roho Mtakatifu njoo anaongozwa roho zetu ku uzima wa milele.

5.Mutu yule anasiriki na kutetemeka kwa ajili ya ukosefu wake hawezi kufundisha wengine, kwa sababu afya ya roho yake inashaharibika.